*Jarida la kituo cha huduma za sheria zanzibar*

Ifanye haki

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*

Iwe shauku

ISSN 0000 - 0000 Toleo Na. 002 Jarida la kila miezi mitatu Aprili - Juni, 2010

## ZLSC yapata ofisi mpya Pemba

**KITUO** cha Huduma za Sheria Zanzibar *(ZLSC)* kimepata ofisi mpya Pemba iliyopo mkabala na ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Pemba.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZLSC, Bw. Iss-haq I. Shariff alisema ofisi mpya ina vyumba vya kutosha kwa matumizi ya ofisi na maktaba.

Alisema uongozi wa ZLSC unatafuta viwanja ili kujenga ofisi zake za kudumu Unguja na Pemba badala ya kuendelea kukodi majengo ya ofisi kwa kipindi kirefu tokea ilipoanzishwa.

ZLSC imeanzishwa mwaka 1992 na ilikuwa ikifanya shughuli zake Unguja tu.

Hata hivyo, ZLSC imepanua shughuli zake na kufungua tawi lake Pemba ili kuwa karibu na wananchi kwa kuwahudumia vizuri.

Miongoni mwa kazi za ZLSC ni kutoa msaada wa kisheria kwa wasiojiweza.

Vile vile ZLSC inaandaa warsha mbali mbali zinazohusiana na mambo ya sheria na kuchapisha ripoti na tafiti za kisheria.

## Habari kwa ufupi

**Kesi ya ubakaji yamalizwa 'kienyeji'**

JUMA Suleiman Kombo (37), mkaazi wa Kibweni, Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, amefikishwa Kituo cha Polisi Bububu kwa tuhuma za kumpa uja mzito msichana (jina linahifadhiwa) kinyume na sheria. Kumbukumbu za Kituo cha Polisi (RB 1493/10) zinaonyesha kwamba kesi hiyo iliripotiwa kituoni hapo lakini taarifa ya awali inaonesha kwamba kesi hiyo ilimalizwa kienyeji bila ya kufikishwa Mahkamani. Kituo bado kinaendelea kufuatilia kwa karibu kesi hiyo.

**Wafanyakazi wa afya wasomeshwa Sheria**

KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (**ZLSC**) kimetoa mafunzo ya Sheria kwa wafanyakazi 28, kati ya hao wanaume 11 na wanawake 17, wa Chuo Cha Afya Mbweni, kwa ajili ya kuwafahamisha haki zao za msingi na wajibu wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa **ZLSC**, Iss-haq I. Shariff alisema kwamba miongoni mwa mada zilizotolewa ni Sheria za Kazi za Zanzibar, misingi ya Katiba na Haki za Binadamu.




*Aliyekuwa Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Bw. Staffan Herrstrom, akizungumza na baadhi ya wawakilishi wa mtandano wa asasi za kiraia zinazojishughulisha na maswali ya haki za watoto katika ukumbi wa mikutano wa Kituo cha Huduma Sheria Zanzibar.*

*Jarida la kituo cha huduma za sheria zanzibar*

Ifanye haki

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*

Iwe shauku

ISSN 0000 Toleo Na. 002 Jarida la kila miezi mitatu Aprili - Juni, 2010

# Mwenyekiti ZLSC atunzwa

**MWENYEKITI** wa Bodi ya Wadhamini wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar *(ZLSC)*, Profesa Chris Maina Peter ametunikiwa zawadi na Chama Cha Wanasheria Tanganyika *(TLS)* kwa juhudi za kuiendeleza fani ya sheria.

Profesa Peter ambaye pia ni mhadhiri mwandamizi wa Kitivo cha Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*) na alikuwa ni mwananchama wa 110 kujiunga *TLS* mwaka wa 1984. *TLS* ina wanachama zaidi ya 2000.

Akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kukabidhiwa zawadi, profesa Peter alisema ataelekeza juhudi zaidi kutoa elimu ya sheria kwa wasiojiweza ili kutetea haki zao zinapovunjwa.

"Ninaumia sana kuona wanyonge wanakosa haki zao kwa kutotambua elimu ya sheria," alisema Profesa Peter ambaye ameandika vitabu kadhaa vinavyotumika katika Vyuo Vikuu vya ndani na nje ya nchi pamoja na kuhariri vitabu mbali mbali vya wasomi mashuhuri wa Afrika Mashariki.

Amekuwa akifundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa zaidi ya miaka 30. Miongoni mwa masomo anayofundisha ni Haki za Binadamu, Sheria za Wakimbizi, Sheria za Kimataifa, Sheria za Bahari, Sheria za Madhara na Sheria za Vitega Uchumi.

Vile vile Profesa Peter amefundisha katika vyuo vikuu mbali mbali vikiwemo Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani, Chuo Kikuu cha Warwick nchini Uingereza, Chuo Kikuu cha Graz nchini Austria na Chuo Kikuu cha Raul Wallenberg nchini Sweden.



***Prof. Chris Maina Peter***

# Waziri ashauri fani ya sheria ikuzwe Zanzibar

**KITUO** Cha Huduma za Sheria Zanzibar (*ZLSC*) kimeshauriwa kutafuta mbinu mbali mbali za kukuza fani ya sheria Zanzibar.

Ushauri huo umetolewa na Waziri wa Nchi (*AR*) Katiba na Utawala Bora, Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban alipokuwa akizindua Jarida la *"Sheria na Haki"* linalotolewa na Kituo kila baada ya miezi mitatu.

Katika uzinduzi huo, Waziri alisema fani ya sheria bado ni changa na lazima ikuzwe kwa madhumuni ya kuhakikisha Utawala wa Sheria na Utawala Bora unaimarika Zanzibar. Alikitaka Kituo kishirikiane na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali ili kuanzisha tena utoaji wa Ripoti za Sheria Zanzibar (*Zanzibar Law Reports).*

Alisema Zanzibar imeshuhudia maendeleo makubwa katika kukuza Utawala Bora na miongoni mwa maendeleo hayo ni kuwepo kwa Muongozao wa Haki za Binadamu na kusambazwa kwa wananchi kwa lengo la kuwaelimisha ili watambue haki zao na wajibu wa kuzifuatilia inapotokezea kuvunjwa.

Aidha Waziri Shaaban alisema Serikali inathamini mchango unaotolewa na Kituo katika maendeleo ya Sheria hatua ambayo imeongeza ufahamu wa elimu ya sheria na kuwawezesha wananchi kufahamu umuhimu wa sheria na kudai haki zao wanapohisi zimevunjwa.

Sambamba na hilo, alisema wafanyakazi wa taasisi mbali mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali zimefaidika na huduma za Kituo.



***Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, Ramadhan Abdalla Shaaban katika uzinduzi wa jarida la Haki na Sheria***